



AITEL END OF TERM 1 2024 ASSESSMENTS

PAPER ONE

END OF TERM ONE, 2024 ASSESSMENTS

LUGHA YA KISWAHILI, PAPER ONE

TIME: 2:30 hours

MAAGIZO; JIBU MASWALI YOTE

1. Kwa ufupi, eleza istilahi zinazo saidia wasomaji kuelewa kazi ya Fasihi.

2. AFRIKA MAMA YETU

Amkeni kila pombe, sasa kumepambambazuka.

Twanyanyaswa kama ng'ombe, hali giza latoweka

Damu moto tujisombe, sote wana Afrika

Bara zima tuungane, tukomboe Afrika.

Kwenye heri au shari, ukombozi tunataka

Ubaguzi ni hatari, ni unyama wa tabaka

Bara zima tuungane, tukomboe Afrika

Bara zima tuungane, tukomboe Afrika

Tukomboe bara letu, Viongozi wasifika
Dumisha umoja wetu nchi huru Afrika
Umoja ni nguo yetu, hatutaki kutengeka
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika.

Sote tunajua vyema, mama yetu Afrika
Tena tumpe uzima, kubwa usiopimika
Kwa kuondoa unyama, wa kusi na vibaraka.
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika.

Vijana tangulioni, mbele bila kugeuka
Misiri hadi kusini, milikeni Afrika
Kaburu na mahaini, kuwatia hekaheka
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika.

Ukoloni mamboleo, na ubwana tumechoka
Wenyeji na wengineo, ni mabomu kufyatuka
Maovu si marejeo, tusirudi tukotoka
Bara zima tuungane, tukomboe Afrika.

Maswali

- (a) Chambua bahari la shairi hili.
- (b) Toa maudhui sita(6) unayopata katika shairi hili .

3(a) Toni ni nini?

- (b) Orodhesha aina mbili za toni
- (c) Orodhesha aina 6(sita) za toni uathiliwa na hisia au hali na mazingira ya mwandishi au mhusika.
- (d). Jadili hisia zinayo muasiri mhusika/mwandishi au msomaji kwa namna ya kuhusika.

4. Soma nathari ifuatayo na kisha ujibu maswali.

Kipsang aliamka akiwa na tele. Alitembea kama hima hadi bafuni. Baada ya kuoga alijizatiti kuvishuka vidato. Aliingia sebuleni na akapata staftahi mezani. Alitabasamu na akaanza kula. Alikuwa akila aliposikia sauti ya mama yake. Alimtazama kumjulia hali. Aah kula polepole mwanangu usiwe na **“haraka haraka haina Baraka”**Mma alisema.

Baada ya Muda mfupi, kipsanga alitoka nyumbani na kuelekea garini. Aliweka Mkoba wake garini na kumsubiri baba yake.

Baba alipoingia kwenye gari aliliasha na kushika fariki kuelekea shulenii.

Baba ongeza kiasi, Kipsanga”alisema”mbona haraka hizi zimezidi unasahau kwamba “**pole pole ndio mwendo?**” baba aliuliza. Walipofika shulenii kipsanga alitoka garini na kutembea **chapuchapu** hadi darasani. Alimkuta mwanafunzi mmoja darasani. Aliketi kwenye dawati lake na baada ya kuweka vitabu vyake dawalini akaanza kuchokoza mwenzake aliyekuwa akiwa akijaribu kusoma. Kijana yule hakutaka kuchezewa na akamwambia Kipsanga amwache.

Kipsang alimwangalia kwa macho makali kama chui. Kijana yule, aliyeitwa Baraka alinyamaza Kimya kingi. Naam Kimya kingi kina msindo mkuu.

Punde si punde, mwalimu aliingia darasani na kuwasuburi wanafunzi wengine waje ‘mbona husomi na unajua kuwa kuna mtihani leo?

Mwalimu alimwuliza kipsang. Tafadhalii soma uelewe kwamba usipoyasikia maneno yangu hatafaulu kamwe. Kwani **asiyesikia la mkuu huvungika mguu**.

Kipsang alitoa kitabu na kujifanya anasoma kumbe ni uongo tu. Akasema kimoyomoyo”**unafikiri mimi ni mjinga/ au unafikiri mimi ni kama ngombe ambaye lazima aonyeshwa maji ndipo anywe”**.

Masikio hayapiti kichwa. Mwalimu aligundua kwamba kipsang hasomi. Akazidi kusihi aache upuuzi. **Mchimba kisima huingia mwenyewe**.

Wanafunzi walifanya mitihani huo. Mwisho wa mhura wa tatu ulikuwa ukikaribia. Wakati ulifika na wazazi walienda na watoto wao kuchua ripoti za watoto wao. Baba yake Baraka alikuwa na furaha tele baada ya kukuta kwamba mtoto wake ndiye aliyekuwa wa mwisho darasani. Kipsang alikuwa hana la kufanya ila kusalimu amri na kusoma kidato hicho tena. Nakwahivyo, **Mpanda ovyo huvuna ovyo.** Kila mtu huvuna alichopanda.

Maswali

- (a) Wew kama mwanafunzi unajifunza nini kutoka kwa methali hii.
- (b) Taja kichwa cha nathari hii ambacho ni methali kisha ueleze maana ya kichwa hicho ukilejelea yaliyomo hadithini
- (c) Taja sifa tatu za kijana Baraka.
- (d) Taja methali tano zinazotumiwa katika nathari hii.
- (e) Umepata hisia gani wewe kama msomaji wa habari hii.
- (f) Mwandishi wa taarifa hii ameonyesha ubingwa/uhodari wowote kukizingatia matumizi ya lugha? Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutumia hoja sita(6).

MWISHO

Prepared by Bwana Johnani
Bamwesigye, bjohnani@gmail.com,
0789216780/0752561101